




JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA MTWARA
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)



Kumb. Na. AC.253/525/01/149

25/07/2024

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Halmashauri ya Wilaya Mtwara inatangaza nafasi za kazi kwa wananchi wenye sifa za kuwa Wasaidizi wa Kumbukumbu kufuatia kupata kibali cha Ajira chenye Kumb.Na. FA.97/288/01/09 cha tarehe 25/06/2024 kama ifuatavyo;

1.0 MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA LA II NAFASI TATU (3).

1.0.1 KAZI NA MAJUKUMU

- i. Kudhibiti upokeaji,uandikishaji wa kumbukumbu/nyaraka
- ii. Kushughulikia maombi ya kumbukumbu/nyaraka kutoka taasisi za serikali
- iii. Kuchambua,kuorodhesha na kupanga kumbukumbu/nyaraka katika makundi kulingana na somo husika (classification and boxing) kwa ajili ya matumizi ya ofisi
- iv. Kuweka/kupanga kumbukumbu/nyaraka katika reki (file racks/cabinet) katika masijala/vyumba vya kuhifadhia kumbukumbu
- v. Kuweka kumbukumbu barua,nyaraka katika mafaili
- vi. Kutafuta kumbukumbu/nyaraka/mafaili yanayohitajiwa na wasomaji
- vii. Kufanyia ukarabati kumbukumbu zilizoharibika
- viii. Kuweka/kupanga kumbukumbu/nyaraka katika vyumba vya kuhifadhia nyaraka

1.0.2 SIFA ZA MWOMBAJI

Awe amehitimu elimu ya kidato cha iv au cha vi

Awe na cheti cha utunzaji wa kumbukumbu stahada/cheti NTA level 6

Kati ka fani ya masijala kutoka vyuo vinavyotambuliwa na serikali,mwenye ujuzi wa kompyuta

1.0.3 MSHAHARA

Kwa kuzingatia ngazi za mishahara ya Watumishi wa Serikali, mshahara utakuwa ni TGS C.1.

MASHARTI YA JUMLA

- i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri wa kuanzia miaka 18 na usiozidi miaka 45 isipokuwa kwa wale tu walioko kazini Serikalini;
- ii. **Waombaji wenye ulemavu wanahamasishwa kutuma maombi na wanapaswa kuainisha kwenye Mfumo wa kuombea ajira ulemavu walionao kwa ajili ya taarifa kwa Sekretarieti ya Ajira Katika Utumishi wa Umma**
- iii. Waombaji wote waambatishe maelezo binafsi yaliyojitosheleza (Detail Curriculum Vitae) yenye anuani inayotumika, namba za simu zinazopatikana na Anuani ya Barua Pepe (E-mail address) pamoja na majina ya wadhamini (Referees) watatu wa kuaminika.
- iv. Waombaji ambao tayari ni Watumishi wa Umma na wamejipatia Sifa zakuingilia katika kada tofauti na walizonazo, wapitische barua zao za maombi yanafasi ya kazi kwa waajiri wao na waajiri wao wajiridhishe ipasavyo.
- v. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detail C.V) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika;
- vi. Maombi yote yaambatane na vyeti vya Elimu na Taaluma vilivyothibitishwa na Mwanasheria/Wakili ambavyo ni vyeti vya Kidato cha Nne au Sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika. **Postgraduate/Degree/Advanced Diploma/Diploma/Certificates, - Cheti cha mtihani wa Kidato cha IV na VI, - Computer Certificate, - Vyeti vya Kitaaluma (Professional Certificate from Respective Boards);**
- vii. "Testmonial", "Provisional Results", "Statement of results", hati ya matokeo ya Kidato cha Nne na Kidato cha Sita (**FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS**) **HAVITAKUBALIWA.**
- viii. Waombaji waliosoma nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na vimethibitishwa na Mamlaka husika (**TCU, NECTA na NACTE**).

- ix. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali kutoka kwa Katibu Mkuu Kiongozi.
- x. Waombaji kazi ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa Umma wasiombe na wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyo katika **Waraka Na. CAC.45/257/01/D/140** wa tarehe **30 Novemba, 2010**.
- xi. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
- xii. Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe **08 Agosti, 2024**.
- xiii. MUHIMU: Kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya elimu, anuani ya barua hiyo ielekezwe kwa:-

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya Mtwara,
S.L.P. 528,
MTWARA.

- xiv. Maombi yote yatumwe kwenye mfumo wa kielektroniki wa Ajira (Recruitment Portal) kupitia anuani ifuatayo; <https://portal.ajira.go.tz/> (Anuani hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Sekretarieti ya Ajira kwa kuingia sehemu iliyoandikwa 'Recruitment Portal').
- xv. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili **HAYATAFIKIRIWA.**

Imetolewa na:



Thomas R. Luambano

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA MTWARA**

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)
MTWARA**